

KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU



MWONGOZO WA MISINGI YA BIASHARA NA HAKI ZA BINADAMU



Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu
Jengo la Jaji Lugakingira
Kijitonyama - Dar es Salaam, S.L.P 75254
Simu: +255 22 2773038/48 , Nukushi: +255 22 2773037
Barua pepe: lhrc@humanrights.or.tz
Tovuti: www.humanrights.or.tz



Utekelezaji wa Mfumo wa Umoja wa Mataifa wa
“Linda, Heshimu na Rekebisha”

Member of
fidh



MWONGOZO WA MISINGI YA BIASHARA NA HAKI ZA BINADAMU

**Utekelezaji wa Mfumo wa Umoja wa
Mataifa wa
“Linda, Heshimu na Rekebisha”**

ANGALIZO

Mtindo uliotumika na uwasilishaji wa taarifa katika kitabu hiki haumaanishi kuwa ni maoni ya aina yoyote ya Sekretarieti ya Umoja wa Mataifa kuhusu hali ya kisheria ya nchi, jimbo, mji au eneo lolote, au la mamlaka zake, au kuhusu uwekaji wa mipaka yake.

Alama za nyaraka za Umoja wa Mataifa zimewekwa katika herufi kubwa pamoja na michoro. Kutajwa kwa mchoro huo kutamaanisha kumbukumbu/rejea ya hati za Umoja wa Mataifa.

HR/PUB/11/04

© 2011

Umoja wa Mataifa

Haki zote za Kimataifa zimehifadhiwa

Na Kutafsiriwa na

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu

Juni, 2015

YALIYOMO

ANGALIZO.....	ii
YALIYOMO.....	iii
DIBAJI.....	v
MUHTASARI.....	vi
UTANGULIZI.....	vii
MADHUMUNI YA TAFSIRI YA MWONGOZO WA MISINGI YA BIASHARA NA HAKI ZA BINADAMU.....	viii
KANUNI ZA JUMLA.....	ix
SURA YA KWANZA.....	1
I. WAJIBU WA SERIKALI KULINDA HAKI ZA BINADAMU.....	1
A. MISINGI MIKUU.....	1
B. KANUNI ZA UTEKELEZAJI.....	3
SURA YA PILI.....	16
II. WAJIBU WA KAMPUNI KUHESHIMU HAKI ZA BINADAMU.....	16
A. KANUNI ZA MSINGI.....	16
B. MISINGI YA UTEKELEZAJI JUKUMU LA SERA.....	21
SURA YA TATU.....	37
III. UFIKIWAJI WA MAREKEBISHO.....	37
A. KANUNI ZA MSINGI.....	37
B. KANUNI ZA UENDESHAJI.....	39

Kijitabu hiki ni tafsiri ya Kiswahili ya Kanuni zinazoongoza Biashara na Haki za Binadamu: Katika Utekelezaji wa mpango wa Umoja wa Mataifa wa “kulinda, kuheshimu na kurekebisha” ulioandaliwa na Mwakilishi Maalum wa Katibu Mkuu kwenye masuala ya Haki za Binadamu na Makapuni Makubwa na Biashara nyingine. Mwakilishi Maalum aliambatanisha kanuni hizi kwenye taarifa yake ya mwisho kwa Baraza la Umoja Mataifa la Haki za Binadamu (A/HRC/17/31) ambayo pia ilijumuisha utangulizi wa kanuni hizi na mtazamo wa jumla wa mchakato ulioongoza utungwaji wake. Baraza la Haki za Binadamu walipitisha Kanuni kupitia Azimio lake namba 17/4 la tarehe 19 Juni 2011

DIBAJI

Baraza la Umoja wa Mataifa la Haki za Binadamu liliidhinisha mwongozo mpya kuhusu uhusiano kati ya biashara na haki za binadamu mnamo Mwaka 2011. Mwongozo ambao kwa mara ya kwanza uliweka misingi ya kimataifa ya kukabiliana na athari mbaya zinazotokana na shughuli za biashara kwenye haki za binadamu.

Mwongozo wa biashara na haki za binadamu umetoa wajibu kwa serikali, mashirika ya kimataifa na makampuni mengine ya biashara kulinda na kuheshimu haki za Binadamu. Mwongozo huu unahusisha mataifa na makampuni yote ya biashara, ya kimataifa na mengine bila kujali ukubwa wao.

Misingi iliyoainishwa kwenye mwongozo inapaswa kutekelezwa pasipo ubaguzi wa aina yoyote, ukizingatia hasa haki na mahitaji ya binadamu. Pia changamoto zinazowakabili watu kutoka makundi mbalimbali yakijamii. Pamoja na mambo mengine, Mwongozo huu ni mawazo yenye mantiki na yakueleweka, hivyo unapaswa kusomwa na mtu mmoja mmoja na kwa pamoja ili kuweza kufanikisha matokeo chanya na yenye tija kwa watu jamii na makampuni ili kuchangia utandawazi endelevu na maisha bora kwa jamii .

MUHTASARI

Kitabu hiki kinatoa mwongozo kwa Serikali pamoja na Makampuni mbali mbali kuhusu namna ya kulinda na kuheshimu haki za binadamu kwa kufuata Misingi ya Umoja wa Mataifa katika biashara na haki za Binadamu.

Katika kitabu hiki, Umoja wa Mataifa umeweka misingi ya utekelezaji kwa serikali pamoja na makampuni katika kulinda na kuheshimu haki za binadamu pasipona ubaguzi wa aina yoyote.

Sura ya kwanza imeainisha wajibu wa Serikali kuweka ulinzi dhidi ya ukiukwaji wa haki za binadamu ndani ya nchi/mamlaka kwa kuchukua hatua stahiki za kuzuia, kuchunguza, kuadhibu na kurekebisha ukiukwaji huo kwa kutunga sera, sheria, kanuni pamoja na utekelezaji wake madhubuti.

Sura ya pili inaelezea wajibu wa mashirika/makampuni kuheshimu haki za binadamu kwa kufuata misingi na kanuni za utekelezaji kuepuka ukiukwaji wa haki za binadamu na kushugulikia athari mbaya za uvunjifu wa haki za binadamu zinazosababishwa na makampuni yao.

Sura ya tatu inaelezea stahiki za watu walioathirika kutokana na uvunjifu wa haki za binadamu uliosababishwa na makampuni. Kwa sehemu ni wajibu wa serikali kulinda haki za binadamu zinazohusiana na biashara zisikiukwe, serikali inapaswa kuchukua hatua zinazofaa kiutawala na kisheria, ili kuhakikisha kwamba walioathirika na uvunjifu wa haki za binadamu wanapatiwa fidia stahiki kutokana na maafa hayo

UTANGULIZI

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu ni shirika lisilo la kiserikali linalotambulika kisheria na linalofanya kazi kwa ushirikiano wa moja kwa moja na jamii. Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kilianzishwa mwaka 1995 kama shirika binafsi, la hiari, lisilotengeneza faida kwa nia ya kugawana na hakifungamani na chama chochote cha siasa.

Kituo hiki kimesajiliwa kama kampuni isiyo na hisa, chini ya Sheria ya Makampuni Sura ya 212 ya sheria za Tanzania. Kituo hiki kilianzishwa kama mradi wa haki za binadamu wa shirika jingine linalojulikana kama Shirika la Elimu ya Sheria Tanzania (TANLET).

Kituo hiki kina sifa ya kipekee kutokana na umahiri wake wa utetezi wa masuala mbalimbali ya haki za binadamu na utoaji wa huduma za msaada wa kisheria. Kituo kinafanya kazi zake nchi nzima ya Tanzania kikiwa na makao yake makuu jijini Dar es Salaam eneo la Kijitonyama. Kituo pia kina ofisi ndogo mkoani Arusha. Vile vile Kituo kina kliniki inayojihusisha na utoaji wa huduma za msaada wa kisheria iliyopo Kinondoni, Dar es Salaam.

Ili kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi Kituo kinafanya kazi zake chini ya kurugenzi tatu. Moja kati ya kurugenzi hizo inashugulika na Kukuza uwezo wa jamii pamoja na Uwajibikaji ikiwemo uwajibikaji wa Makampuni.

Miongoni mwa shuguli za idara hii ni pamoja na kuongeza msukumo kwa makampuni ya biashara kuzingatia haki za binadamu, kwa mfano haki ya mazingira safi na salama, haki za ajira na haki za ardhi katika shughuli zake za kila siku. Lengo kuu likiwa ni kuhakikisha kunakuwepo uwajibikaji wa makampuni katika kuheshimu haki za binadamu.

MADHUMUNI YA TAFSIRI YA MWONGOZO WA MISINGI YA BIASHARA NA HAKI ZA BINADAMU

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) kimetafsiri mwongozo wa misingi ya biashara na haki za binadamu kwa lugha nyepesi ya kiswahili kwa lengo la kujenga uelewa wa jamii ya watanzania na makampuni kwa ujumla juu ya kanuni zilizoinishwa na Umoja wa Mataifa katika biashara na uzingatiaji wa haki za binadamu.

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kinatambua umuhimu wa kutafsiri mwongozo huu kwa nia ya kuufikisha kwa kikamilifu kwa wananchi, serikali na makampuni ili waweze kueleweka kwa urahisi na kurahisisha utekelezaji wake.

Azma hii muhimu itafikiwa kwa kanuni hizi zilizotafsiriwa kwa lugha nyepesi ya Kiswahili kwa wananchi wote kuzisoma na kuzielewa ili kutambua haki zao na kuzidai pale zinapo vunjwa. Pia watendaji wa Serikali na Makampuni kufahamu wajibu wao kama ulivyoainishwa kwenye kanuni hizi ili kusimamia na kutekeleza yaliyoainishwa kwenye kanuni kwa maendeleo endelevu na ulinzi wa haki za binadamu.

KANUNI ZA JUMLA

Kanuni hizi ongozi zimejikita katika kutambua;

- a) Wajibu uliopo wa Serikali kuheshimu, kulinda na kutekeleza haki za binadamu na misingi mikuu ya uhuru.
- b) Jukumu la makampuni ya kibiashara kuwa na vyombo mahsusi vyenye kutekeleza majukumu maalum yanayopaswa kuzingatia sheria zote zinazohusika na kuheshimu haki za binadamu.
- c) Uhitaji wa haki na wajibu kulinganishwa ipasavyo na malipo yanayofaa kutolewa pale zinapokiukwa.

Kanuni hizi zinahusu nchi zote na makampuni yote ya biashara yawe yakimataifa au vinginevyo bila kujali iwapo ni makubwa au madogo , sekta zao, yalipo na anayemiliki na hata mifumo yake.

Kanuni hizi hazi na budi kueleweka kama mtiririko mzima na zinatakiwa kusomwa moja moja na hata kiujumla, kwa kuzingatia madhumuni yake ya kuendeleza viwango na tabia ya biashara na haki za binadamu ili kupata matokeo yatakayogusa mtu binafsi au jamii, ili kuchangia katika utandawazi endelevu wa kijamii.

Kanuni hizi hakipaswi kueleweka kama vile zinaanzisha wajibu mpya katika sheria za kimataifa au kuwa zinapunguza au kushusha hadhi ya wajibu wowote wa kisheria ambao nchi ilishaupokea au inawajibika kupitia sheria za kimataifa za haki za binadamu.

Kanuni hizi zinapaswa kutekelezwa katika hali isiyokuwa ya kibaguzi, zikizingatia haki na mahitaji pamoja na changamoto zinazowakabili watu binafsi kutoka katika makundi au jumuiya zinazoweza kuwa katika hatari kuu za kuwa pembezoni au katika mazingira hatarishi na kutilia maanani hatari mbalimbali zinazoweza kuwakuta wanawake na wanaume



SURA YA KWANZA

I. WAJIBU WA NCHI KULINDA HAKI ZA BINADAMU

A. MISINGI MIKUU

- 1. Serikali zina wajibu wakutoa ulinzi dhidi ya ukiukwaji wa haki za binadamu ndani ya nchi zao na/au mamlaka za kisheria, ikiwa ni pamoja na makampuni ya biashara. Kufanya hivyo kunahitaji kuchukua hatua stahiki za kuzuia, kuchunguza, kuadhibu na kurekebisha ukiukwaji huo kwa kutumia Sera, Sheria, Kanuni na maamuzi madhubuti ya kisheria.**

Maoni

Sheria za Kimataifa za haki za binadamu zimetoa wajibu kwa serikali kuheshimu, kulinda na kutekeleza haki za binadamu za watu binafsi ndani ya nchi zao na/au mamlaka za kisheria. Hii ni pamoja na wajibu wa kutoa ulinzi dhidi ya ukiukwaji wa haki za binadamu unaofanywa na mtu dhidi ya mwingine, ikiwa ni pamoja na makampuni ya biashara.

Wajibu wa serikali kulinda haki za binadamu ni kiwango au kipimo katika utekelezaji wake. Kwa hiyo, Mataifa hayawajibiki moja kwa moja katika ukiukwaji wa haki za binadamu unaofanywa na watendaji kwenye sekta binafsi. Hata hivyo, serikali zinaweza kukiuka wajibu wao wa sheria za kimataifa za haki za binadamu pale zinapoweza kuhusishwa na ukiukwaji huo, au pale zinaposhindwa kuchukua hatua stahiki kuzuia, kuchunguza, kuwaadhibu na kurekebisha ukiukwaji

wa watendaji katika sekta binafsi. Ingawa serikali kwa ujumla zina hiari kuamua juu ya hatua hizi, ni lazima zifikirie kiwango kamili cha hatua zinazoruhusiwa kuzuia na kurekebisha, ikiwa ni pamoja na sera, sheria, kanuni na maamuzi ya kisheria. Serikali zina wajibu pia wa kulinda na kukuza utawala wa sheria, ikiwa ni pamoja na kuchukua hatua za kuhakikisha usawa mbele ya sheria, haki katika utekelezaji wa sheria, uwajibikaji wa kutosha, kutoa uhakika wa kisheria na uwazi katika taratibu za kisheria.

Sura hii inalenga kuonyesha hatua zinazoweza kuchukuliwa ili kuzuia wakati Sura ya Tatu inaelezea hatua zinazoweza kuchukuliwaa katika utatuzi.

2. Serikali zinapaswa kuweka bayana matarajio ambayo makampuni yote ya biashara yaliyo katika nchi/au mamlaka zao za kisheria yanapaswa kuheshimu haki za binadamu katika shughuli zao zote.

Maoni

Kwa wakati uliopo, Serikali hazihitajiki kwa mujibu wa sheria za kimataifa za haki za binadamu kusimamia shughuli za biashara nje ya mipaka ya nchi au /mamlaka zao za kisheria. Wala kwa ujumla hawakatazwi kufanya hivyo, ili mradi mamlaka ya kisheria iwe inatambuliwa. Kwa mipaka hii, baadhi ya vyombo vya usimamizi wa mikataba ya haki za binadamu vinapendekeza kwamba serikali pale zilipo zichukue hatua za kuzuia ukiukwaji unaofanywa na makampuni ya biashara kutoka nchini kwao, yakiwa nje ya nchi hizo.

Kuna sababu nzito za kiseria zinazofanya serikali za nchi yanakotokea makampuni ya biashara kuweka wazi matarajio ya biashara hizo

kuheshimu haki za binadamu wakiwa nje ya nchi, hasa pale ambapo serikali yenyewe inashiriki au kusaidia biashara hizo. Sababu hizi ni pamoja na kuhakikisha, kuaminika kwa makampuni ya biashara kwa kutoa maagizo madhubuti na thabiti, na kulinda sifa ya nchi yenyewe.

Serikali zimetumia mbinu mbalimbali katika suala hili. Baadhi ni hatua za ndani zinazoweza kutumika hata nje ya mipaka ya nchi. Mifano ya mbinu hizo ni pamoja na; masharti ya makampuni Tazunguza kutoa taarifa juu ya shughuli za biashara nzima kimataifa; vyombo vya kimataifa vya sheria nyepesi kama vile Miongozo kwa Makampuni ya Kimataifa ya Shirika la Ushirikiano na Maendeleo ya Uchumi; na viwango vya utendaji vinavyohitajika na taasisi zinazotoa msaada kwa uwekezaji nje ya nchi. Mbinu nyingine ni sheria na utekelezaji nje ya nchi wa sheria za nchi moja kwa moja. Hii ni pamoja na mfumo wa makosa ya jinai ambao unaruhusu mashtaka yanayohusisha utafida wa mkosaji bila kujali lilipotendewa kosa hilo. Mambo mbalimbali yanaweza kuchangia mtazamo na uhalali wa hatua za Nchi', kwa mfano iwapo yanatokana na makubaliano ya kimataifa.

B. KANUNI ZA UTEKELEZAJI

KAZI ZA UDHIBITI NA SERA ZA NCHI KWA UJUMLA

- 3. Ili kutimiza wajibu wao wa kulinda, Serikali zinatakiwa:**
 - (a) Kuhimiza utekelezaji wa sheria ambazo zina lengo la, au zina uwezo wa, kuyataka makampuni ya biashara kuheshimu haki za binadamu, na kwa vipindi maalum kutathmini utoshelevu wa sheria hizo na kushughulikia mapungufu yoyote;**
 - (b) Kuhakikisha kuwa sheria nyingine na sera**

zinazosimamia uundaaji na operesheni zinazoendelea za makampuni ya biashara, kama vile sheria ya makampuni, hazizuii bali zinawezesha makampuni ya biashara kuheshimu haki za binadamu;

- (c) Kutoa mwongozo madhubuti kwa makampuni ya biashara ya namna yanavyoweza kuheshimu haki za binadamu katika shughuli zao;**
- (d) Kuhamasisha, na pale inapobidi, kuhitaji makampuni ya biashara kuwasilisha namna yanavyo shughulikia athari za operationi zao kwa haki za binadamu na jinsi wanavyokabiliana nazo.**

Maoni

Serikali za nchi zisidhani kuwa biashara wakati wowote hupendelea, au hufaidika kutokana na serikali kutokuchukua hatua. Seikali zinapaswa kufikiria hatua bora mchanganyiko kitaifa na kimataifa na za lazima na zile za hiari ili kukuza makampuni ya biashara kuheshimu haki za binadamu.

Kushindwa kutekeleza sheria zilizopo ambazo moja kwa moja au vinginevyo husimamia makampuni ya biashara kuheshimu haki za binadamu mara nyingi ni mapungufu makubwa kisheria katika utendaji wa serikali. Sheria hizo zinaweza kuwa kwenye nyanja mbalimbali kama kutokubaguliwa na sheria za kazi, mazingira, mali, faragha na sheria ya kupambana na rushwa. Kwa hiyo, ni muhimu kwa serikali kuona kama sheria hizo kwa sasa zinatekelezwa kikamilifu, na kama sivyoy, kwa nini iwe hivyo na ni hatua gani zinaweza kuchukuliwa kurekebisha hali hiyo.

Ni muhimu pia kwa serekali kutathmini iwapo sheria hizi zina ubora muhimu kwa kuzingatia hali ilivyo sasa na kama, pamoja na sera husika, zinaweka mazingira yanayoendeleza makampuni ya biashara kuheshimu haki za binadamu. Kwa mfano, ufafanuzi zaidi katika baadhi ya maeneo ya sheria na sera, kama zile zinazosimamia utoaji wa ardhi, ikiwa ni pamoja na haki zinazohusu umiliki au matumizi ya ardhi, mara nyingi ni muhimu kuwalinda wenye haki pamoja na makampuni ya biashara.

Sheria na sera zinazosimamia uundwaji na uendeshaji wa makampuni ya biashara, kama vile sheria za makampuni na sheria za hifadhi, moja kwa moja zinaunda mwenendo au tabia za biashara. Hata hivyo athari zake kwa haki za binadamu bado hazieleweki vizuri. Kwa mfano, sheria ya makampuni na hifadhi haiko wazi juu ya makampuni na wasimamizi wao wanachoruhusiwa kufanya, achilia mbali kile wanachowajibika kufanya, kuhusiana na haki za binadamu. Sheria na sera katika eneo hili zinapaswa kutoa mwongozo wa kutosha ili kuyawezesha makampuni ya biashara kuheshimu haki za binadamu, kwa kuzingatia majukumu ya kimuundo ya utawala yaliyopo kama vile bodi za makampuni

Mwongozo kwa makampuni ya biashara kuheshimu haki za binadamu uonyeshe matokeo yanayotarajiwa na usaidie kuhabarisha juu ya matokeo chanya ya kuingwa. Mwongozo utoe ushauri juu ya njia sahihi, ikiwa ni pamoja na juhudi zinazostahili kufanywa kulinda haki za binadamu, na jinsi ya kuangalia kikamilifu masuala ya jinsia, mazingira magumu na/au kubaguliwa, kutambua changamoto maalum ambazo zinaweza kuwakabili wazawa, wanawake, taifa au kabila, dini na lugha za watu wachache, watoto, watu wenye ulemavu, na wafanyakazi wahamiaji na familia zao.

Taasisi za kitaifa za haki za binadamu ambazo huzingatia Kanuni za Paris, zina jukumu muhimu katika kuzisaidia Nchi kubaini iwapo sheria husika zinaendana na wajibu wao wa kulinda haki za binadamu na kwamba zinatekelezwa kikamilifu, na kutoa mwongozo juu ya haki za binadamu pia kwa makampuni ya biashara na watendaji wengine wasio wa Serikali.

Mawasilisho ya makampuni ya biashara ya namna yanavyoshughulikia matokeo hasi dhidi ya haki za binadamu yanaweza kushirikisha kwa njia isiyo rasmi wadau walioathirika hadi utoaji rasmi wa taarifa kwa umma. Uhamasishaji wa serikali, au pale inapobidi, kuwepo kwa masharti ya utoaji taarifa hizo ni muhimu katika kukuza kuheshimiwa kwa haki za binadamu na makampuni ya biashara. Motisha za kutoa taarifa za kutosha zinaweza kuwa pamoja na masharti ya kuweka uzito utoaji binafsi wa taarifa kama ikibidi kuchukua hatua yoyote ya kimahakama au kiutawala. Sharti la kutoa taarifa linaweza kuwa mwafaka hasa pale ambapo aina ya shughuli za biashara au mazingira yauendeshaji yanahatarisha kwa kiasi kikubwa haki za binadamu. Sera au sheria katika eneo hili zinaweza kufafanua vizuri taarifa gani ya biashara na jinsi gani itolewe, ili kuhakikisha upatikanaji na usahihi wa taarifa.

Ufafanuzi wa nini kiunde taarifa ya kutosha inapaswa kuzingatia hatari ambayo taarifa inaweza kusababisha kwenye ulinzi na usalama wa watu na miundo; mahitaji ya kisheria ya usiri wa biashara; na tofauti za ukubwa na muundo wa makampuni tofauti tofauti.

Masharti ya kutoa taarifa za kifedha yafafanue kwamba athari za haki za binadamu kwa baadhi ya mambo yanaweza kuwa ya “maana” au “muhimu” kwa mafanikio ya kiuchumi kwenye makampuni ya biashara.

KIUNGO CHA DOLA NA BIASHARA

- 4. Serikali zinapaswa kuchukua hatua za ziada kutoa ulinzi dhidi ya ukiukwaji wa haki za binadamu unaofanywa na makampuni ya biashara na hasa yale yanayomilikiwa au kudhibitiwa na Serikali, au yale yanayopata msaada mkubwa na huduma kutoka kwa mawakala wa Serikali kama vile mawakala wa mikopo ya usafirishaji nje na bima ya uwekezaji rasmi au mawakala wa dhamana, na pale inapofaa kuhitaji juhudi zinazostahili katika haki za binadamu.**

Maoni

Nchi moja moja ndizo zenye wajibu mkuu chini ya sheria za kimataifa za haki za binadamu, na kwa pamoja ni wadhamini wa utawala wa haki za binadamu kimataifa. Pale ambapo kampuni ya biashara inasimamiwa na serikali au ambapo matendo yake yanaweza kuhusishwa vinginevyo na Serikali, ukiukwaji wa haki za binadamu unaofanywa na kampuni hiyo ya biashara unaweza kuangaliwa kama uvunjifu wa sheria za kimataifa za nchi yenyewe. Aidha, kadri kampuni ya biashara inavyokuwa karibu zaidi na Serikali, au kadri inavyotegemea zaidi mamlaka ya kisheria au msaada wa walipa kodi, ndivyo kadri sera ya nchi inavyokuwa na nguvu kuhakikisha kwamba kampuni ya biashara inaheshimu haki za binadamu.

Pale ambapo nchi humiliki au kusimamia makampuni ya biashara, huwa na uwezo mkubwa zaidi katika madaraka yao kuhakikisha kwamba sera, sheria na kanuni husika kuhusu kuheshimu haki za binadamu zinazingatiwa. Menejimenti ya juu ambayo kwa kawaida hutoa taarifa kwa mawakala na idara husika za serikali zina wigo mkubwa wa kuangalia na kusimamia, pamoja na kuhakikisha haki

za binadamu zinatekelezwa. (Makampuni haya pia yanawajibika kuheshimu haki za binadamu, kama ilivyo elezewa kwenye Sura ya Pili)

Mawakala mbalimbali yanayohusiana rasmi au isivyo rasmi wanaweza kutoa msaada na huduma kwenye shughuli za biashara. Hizi ni pamoja na mawakala wa mikopo ya usafirishaji nje, bima ya uwekezaji rasmi au mawakala wa dhamana, mawakala wa maendeleo na taasisi za fedha za maendeleo. Pale ambapo mawakala hawa hawazingatii wazi athari mbaya za sasa na zile zenye uwezekano wa kutokea kwa haki za binadamu kwa makampuni ya walengwa, hujiweka hatarini katika sifa zao, kifedha, kisiasa na pengine kisheria kwa ajili ya kusaidia madhara yoyote kama hayo, na yanaweza kuongeza changamoto za haki za binadamu zinazoikabili nchi inayowapokea.

Kutokana na hatari hizi, serikali lazima zihimise na, pale inapofaa, zinahitaji kuchukua juhudi zinazostahili za haki za binadamu toka kwa mawakala wenyewe na kwa makampuni ya biashara au miradi inayopata misaada kutoka kwao. Sharti la juhudi zinazostahili kwa haki za binadamu linaweza kufaa zaidi pale ambapo aina ya shughuli za biashara au mazingira ya uendeshaji yanahatarisha kwa kiasi kikubwa haki za binadamu.

- 5. Serikali za nchi zinapaswa kufanya usimamizi wa kutosha ili kukidhi wajibu wao wa kimataifa wa haki za binadamu wanapofanya mikataba, au kutunga sheria kwa makampuni ya biashara ili kutoa huduma zinazoweza kufanikisha upatikanaji wa haki za binadamu.**

Maoni

Serikali haziachi kutekeleza majukumu yake kwenye sheria za kimataifa za haki za binadamu wanapobinafsisha utoaji wa huduma ambazo zinaweza kufanikisha upatikanaji wa haki za binadamu. Kushindwa kwa serikali ya nchi husika kuhakikisha kuwa makampuni ya biashara yanayotoa huduma na kufanya kazi kwa kufuata wajibu wa nchi wa kuheshimu haki za binadamu, kunaweza kusababisha athari kwenye sifa na hata kisheria kwa nchi husika. Ni muhimu, kuweco kwa mikataba husika ya huduma au sheria za kuwezesha kufafanua matarajio ya nchi kwa makampuni haya kuheshimu haki za binadamu. Serikali zihakikishe kwamba zinaweza zisimamia kwa ufanisi shughuli za makampuni, ikiwa ni pamoja na kutoa taratibu binafsi za ufuatiliaji na uwajibikaji wa kutosha.

6. Nchi zikuze heshima ya haki za binadamu kwenye makampuni ya biashara ambayo hufanya nayo makubaliano ya kibiashara.

Maoni

Serikali za nchi hufanya makubaliano ya kibiashara ya aina mbalimbali na makampuni ya biashara, na si tu kwa shughuli za manunuzi. Hii huzipa Serikali moja moja na kwa pamoja fursa za kipekee kujenga uelewa na kuheshimu haki za binadamu kwa makampuni hayo, ikiwa ni pamoja na masharti kwenye mikataba, kwa kuzingatia majukumu husika ya nchi chini ya sheria za kitaifa na kimataifa.

KUSAIDIA MAKAMPUNI YA BIASHARA KUHESHIMU HAKI ZA BINADAMU KATIKA MAENEO YENYE MIGOGORO

- 7 Kwa sababu hatari ya ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu inaongezeka katika maeneo yaliyoathiriwa na migogoro, Serikali zisaidie kuhakikisha kwamba makampuni ya biashara yanayofanya kazi katika mazingira hayo hayahusishwi na ukiukwaji huo, ikiwemo kwa:
- (a) Kushirikisha makampuni ya biashara katika hatua za mwanzo kadri iwezekanavyo ili kuwasaidia kutambua, kuzuia na kupunguza hatari za shughuli zao na mahusiano ya kibiashara yanayohusiana na haki za binadamu;
 - (b) Kutoa misaada ya kutosha kwa makampuni ya biashara ya kutathmini na kushughulikia hatari zinazoongezeka za ukiukwaji wa haki, kutoa kipaumbele kwenye ukatili wa kijinsia na ukatili wa kingono;
 - (c) Kutokutoa fursa za msaada na huduma za serikali kwa kampuni ya biashara inayojihusisha na ukiukwaji wa haki za binadamu na iliyokataa kushirikiana katika kushughulikia hali hiyo;
 - (d) Kuhakikisha kwamba sera, sheria, kanuni zilizopo na hatua za utekelezaji zinafaa kushughulikia hatari ya uhusishwaji wa biashara katika ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu.

Maoni

Baadhi ya ukiukwaji mbaya kabisa wa haki za binadamu unaoshirikisha biashara hutokea kunapokuwa na migogoro juu ya udhibiti wa eneo, rasilimali au Serikali yenyewe ambapo mfumo wa haki za binadamu hauwezi kutarajiwa kufanya kazi kama ilivyokusudiwa.

Biashara zinazowajibika zinazidi kutafuta mwongozo kutoka kwa Serikali kuhusu jinsi ya kuepuka kuchangia madhara kwa haki za binadamu katika mazingira hayo magumu. Mbinu za ubunifu na vitendo zinahitajika. Hasa, ni muhimu kuwa makini na hatari ya ukatili wa kingono na kijinsia, ambao hasa huongezeka wakati wa vita.

Ni muhimu kwa mataifa yote kushughulikia masuala mapema kabla ya hali iliyopo haijazidi kuwa mbaya. Katika maeneo yaliyoathirika kwa migogoro, Serikali ya nchi “mwenyeji” inaweza kushindwa kulinda haki za binadamu kiasi cha kutosha kutokana na kutokuwa na udhibiti mzuri. Pale makampuni makubwa ya kimataifa yanapohusishwa, nchi zao walipotoka zinakuwa na majukumu ya kusaidia makampuni hayo na nchi wenyeji kuhakikisha kwamba biashara hazihusishwi na ukiukwaji wa haki za binadamu, wakati nchi jirani zinaweza kutoa msaada muhimu wa ziada.

Ili kufikia uthabiti mkubwa wa sera na kusaidia makampuni ya biashara kiasi cha kutosha katika hali kama hizo, nchi wenyeji lazima ziendelee ushirikiano wa karibu kati ya mashirika ya msaada wa maendeleo, wizara za kigeni na biashara, na taasisi za fedha za usafirishaji nje katika miji yao mikuu na ndani ya balozi zao, hali kadhalika kati ya makampuni hayo na watendaji wa Serikali mwenyeji; kuunda viashiria vya onyo la mapema kutahadharisha vyombo vya serikali na makampuni ya biashara na matatizo; na uambatanishe matokeo sahihi

ya makampuni yoyote kushindwa kushirikiana katika mazingira haya, ikiwa ni pamoja na kuwanyima au kuondoa msaada au huduma za umma zilizopo, au pale ambapo hilo haliwezekani, kuwanyima msaada na huduma zao za baadaye.

Nchi zitoe onyo kwa makampuni ya biashara yaliyo katika hatari zaidi ya kuhusishwa na ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu katika maeneo yaliyoathirika na migogoro. Wanapaswa kutathmini kama sera, sheria, kanuni zao na hatua za utekelezaji zinashughulikia kikamilifu ongezeko hili la hatari, ikiwa ni pamoja na kuweka masharti ya juhudi za biashara zinazostahili, za haki za binadamu. Pale wanapobaini mapungufu, Nchi zinapaswa kuchukua hatua muafaka kukabiliana nayo. Hii inaweza kujumuisha kuchunguza dhima ya madai, utawala au makosa ya jinai kwa makampuni yaliyofanya au kuchangia ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu, ambayo yanaishi au kufanya kazi katika nchi na/au mamlaka zao. Vile vile, Nchi zifikirie mbinu za kimataifa za kuzuia na kushughulikia vitendo hivyo, pamoja na mipango ya pamoja madhubuti ya msaada.

Hatua hizi zote ni pamoja na wajibu wa Nchi chini ya sheria ya kimataifa ya ubinadamu katika hali za migogoro ya silaha, na chini ya sheria ya kimataifa ya makosa ya jinai.

KUHAKIKISHA UTHABITI WA SERA

- 8. Nchi zinapaswa kuhakikisha kuwa idara za serikali, mawakala na taasisi nyingine za Serikali ambazo hutengeneza utaratibu wa biashara zinafahamu na kutekeleza majukumu ya Nchi ya haki za binadamu, wakati wanapotimiza wajibu wao mbalimbali, ikiwa ni pamoja na kuwapatia taarifa muhimu, mafunzo na msaada.**

Maoni

Hakuna mgongano kati ya majukumu ya kimataifa, ya haki za binadamu na sheria na sera wanazoweka ambazo huunda utaratibu wa biashara. Hata hivyo, wakati mwingine, inabidi Nchi zifanye maamuzi magumu ya kusawazisha ili kuoanisha mahitaji mbalimbali ya jamii. Ili kufikia uwiano sahihi, Nchi zinatakiwa kutumia mbinu pana kusimamia biashara na mpango wa haki za binadamu, kwa lengo la kuhakikisha msimamo wima na wa mlalo wa sera za ndani.

Msimamo wima wa sera unahusu Nchi kuwa na sera, sheria na taratibu muhimu ili kutekeleza majukumu yake ya sheria za kimataifa za haki za binadamu. Msimamo wa sera mlalo humaanisha kusaidia na kuziandaa katika ngazi za kitaifa na kwenye ngazi za chini, zinazoandaa utaratibu wa biashara ikiwa ni pamoja na zile zinazohusika na sheria za makampuni na kanuni za hifadhi, uwekezaji, mikopo ya kusafirisha nje na bima, biashara na kazi kufahamishwa na kutenda katika njia zinazooana na majukumu ya Serikali ya haki za binadamu.

- 9. Nchi zidumishe nafasi zake zakutumia sera za ndani kutimiza majukumu yake ya haki za binadamu wakati wanapofuatilia malengo ya kiseri yanayohusisha Nchi nyingine au Makampuni ya biashara, kama kwa kutumia makubaliano ya uwekezaji na mikataba.**

Maoni

Mikataba ya kiuchumi iliyoamuliwa na serikali ya nchi, ama pamoja na serikali ya nchi nyingine au na makampuni ya biashara kama vile mikataba ya uwekezaji ya pande mbili, makubaliano au mikataba ya miradi ya uwekezaji hujenga fursa za uchumi kwa nchi. Lakini inaweza

pia kuathiri ufanyaji maamuzi wa Serikali wa kutumia sera zake za ndani ili kuleta maendeleo. Kwa mfano, masharti ya makubaliano ya uwekezaji ya kimataifa yanaweza kuzizuia Nchi kutekeleza kikamilifu sheria mpya za haki za binadamu, au kuziweka katika hatari ya maamuzi ya kisheria ya kimataifa ikiwa watafanya hivyo. Kwa hiyo, Nchi zihakikishe kwamba zinadumisha uwezo wa kutosha wa sera na udhibiti wa kulinda haki za binadamu chini ya masharti ya mikataba hiyo, huku ikitoa ulinzi muhimu wa mwekezaji.

10. Nchi, zikiwa zinatenda kama wanachama wa taasisi za kimataifa zinazoshughulikia masuala yanayohusiana na biashara, zinatakiwa:

- (a) Zihakikishe kuwa taasisi hizo hazizuii uwezo wa Nchi wanachama wao;
- (b) Kutimiza wajibu wao wa kulinda wala kuzuia makampuni ya biashara kuheshimu haki za binadamu;
- (c) Kuhimiza taasisi hizo, ndani ya madaraka na uwezo wao ipasavyo, kukuza haki za binadamu kwenye biashara na zinapohitajika, kuzisaidia Nchi kutimiza wajibu wao wa kulinda ukiukwaji wa haki za binadamu unaofanywa na makampuni ya biashara, ikiwa ni pamoja na kuzipatia misaada ya kiufundi, kujenga uwezo na kuinua ufahamu;
- (d) Kutumia Mwongozo huu kukuza uelewa wa pamoja na kuendeleza ushirikiano wa kimataifa katika usimamizi wa biashara na changamoto za haki za binadamu.

Maoni

Sera za wazi na zinazoeleweka pia zinahitajika katika ngazi ya kimataifa, pamoja na pale ambapo nchi hushiriki katika taasisi za

kimataifa zinazoshughulikia masuala yanayohusiana na biashara, kama vile taasisi za biashara za kimataifa na za fedha.

Nchi huhifadhi wajibu wake kwenye sheria ya kimataifa ya haki za binadamu wanaposhiriki katika taasisi hizo.

Kujenga uwezo na kukuza ufahamu kupitia taasisi hizo kunawezesha kutekeleza jukumu muhimu katika kusaidia Mataifa yote kutimiza wajibu wao wa kulinda, ikiwa ni pamoja na kuyawezesha kubadilishana taarifa kuhusu changamoto na njia bora za kulinda, hivyo kukuza mbinu thabiti zaidi.

Hatua za pamoja kupitia taasisi za kimataifa zinaweza kusaidia nchi kusawazisha shughuli zinazohusiana na biashara na kuheshimu haki za binadamu, lakini ni lazima kufanya hivyo kwa kuongeza utendaji wa mashirika yaliyozorota. Ushirikiano kati ya Mataifa, taasisi za kimataifa na wadau wengine unaweza kusaidia utekelezaji wa majukumu ya muhimu.

Mwongozo huu hufanya rejea ya kawaida katika suala hili, na unaweza kutumika kama msingi muhimu kwa ajili ya kuleta mabadiliko chanya ambayo yatazingatia wajibu na majukumu ya wadau wote muhimu.

SURA YA PILI

II. WAJIBU WA KAMPUNI KUHESHIMU HAKI ZA BINADAMU

A. KANUNI ZA MSINGI

- 11. Makampuni ya biashara yanapaswa kuheshimu haki za binadamu. Hii ina maana yanapaswa kuepuka kukiuka haki za binadamu na kushughulikia athari mbaya za haki za binadamu wanazohusika nazo.**

Maoni

Wajibu wa kuheshimu haki za binadamu ni kiwango cha kimataifa cha mwenendo unaotarajiwa kwa makampuni yote ya biashara popote pale yanapofanya kazi kutimiza. Kila nchi ina uwezo na/au nia yake yenyewe ya kutimiza majukumu yake ya haki za binadamu, wala haipunguzi wajibu huo na ni zaidi ya uzingatiaji wa sheria na kanuni za kitaifa zinazolinda haki za binadamu.

Kushughulikia athari mbaya za haki za binadamu inahitaji hatua za kutosha kuchukuliwa kuzuia, kukabiliana ,na kuboresha pale ambapo inafaa kufanya hivyo.

Makampuni ya biashara yanaweza kutekeleza ahadi/majukumu au shughuli nyingine kusaidia na kuendeleza haki za binadamu na kuimarisha kuchangia upatikanaji wa haki za binadamu. Lakini hii haifidii kushindwa kuheshimu haki za binadamu katika shughuli zao.

Makampuni ya biashara hayapaswi kudhoofisha uwezo wa Nchi kutimiza majukumu yake ya haki za binadamu, ikiwa ni pamoja na vitendo ambavyo vinaweza kudhoofisha uadilifu wa michakato ya kimahakama.

- 12. Wajibu wa makampuni ya biashara kuheshimu haki za binadamu inahusu haki za binadamu zinazotambuliwa kimataifa, hata zile zilizo kwenye kiwango cha chini, kama zilivyoonyeshwa katika Sheria na kanuni za Kimataifa za Haki za Binadamu juu ya haki za msingi zilizowekwa katika Azimio la Shirika la Kazi Duniani juu ya Kanuni za Msingi na Haki za Kazi.**

Maoni

Kwa kuwa makampuni ya biashara yanaweza kusababisha athari juu ya wigo mzima wa haki za binadamu kimataifa, wajibu wao unahusu kuheshimu haki zote hizo. Kivitendo, baadhi ya haki za binadamu zinaweza kuwa katika nafasi kubwa zaidi ya kuathirika kuliko nyingine kulingana na shughuli au mazingira fulani, na hivyo itategemea kiwango cha tahadhari kilichowekwa. Hata hivyo, hali inaweza kubadilika, hivyo haki zote za binadamu inabidi ziwe zinapitiwa kila baada ya muda fulani.

Orodha inayoaminika ya haki za msingi za binadamu, inayotambuliwa kimataifa imo katika Sheria ya Kimataifa ya Haki za Binadamu (yenye Azimio la Kimataifa la Haki za Binadamu na vyombo vikuu ambavyo vimeweka katika mpango ulio wazi: Mkataba wa Kimataifa kuhusu Haki za Kiraia na Kisiaa na Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiuchumi, Kijamii na Kitamaduni), pamoja na kanuni kuhusu haki za msingi katika mikataba nane ya msingi ya Shirika la Kazi Duniani

kama inavyoelezwa katika Azimio kuhusu Kanuni na Haki za Msingi Kazini. Kanuni hizi ni vigezo ambavyo watendaji wengine huvitumia kutathmini athari za haki za binadamu zinazosababishwa na makampuni ya biashara. Jukumu la makampuni ya biashara kuheshimu haki za binadamu ni tofauti na masuala ya dhima ya kisheria na utekelezaji, ambao umefafanuliwa kwa kiasi kikubwa na vifungu vya sheria za kitaifa katika mamlaka tofauti.

Kulingana na hali halisi, makampuni ya biashara yanaweza kuhitaji kufikiria vigezo vya ziada. Kwa mfano, makampuni yanapaswa kuheshimu haki za binadamu za watu walio katika makundi maalum au watu wanaohitaji uangalizi maalum, ambapo haki zao zinaweza kuathirika. Katika uhusiano huu, vyombo vya Umoja wa Mataifa vimefafanua zaidi juu ya haki za wazawa; wanawake; makundi ya dini na lugha za walio wachache kitaifa au kikabila; watoto; watu wenye ulemavu; na wafanyakazi wahamiaji na familia zao. Kadhalika, katika hali ya vita, makampuni yanapaswa kuheshimu viwango vya sheria za kivita za kimataifa na kitaifa

- 13. Wajibu wa kuheshimu haki za binadamu huyataka makampuni ya biashara:**
- (a) Kuepuka kusababisha au kuchangia katika athari mbaya za haki za binadamu kupitia shughuli zao wenyewe, na kushughulikia athari hizo zinapotokea;**
 - (b) Kuzuia au kupunguza athari mbaya kwa haki za binadamu ambazo zinahusiana moja kwa moja na shughuli zao, bidhaa au huduma kwenye mahusiano yao ya biashara, hata kama wao hawachangii katika athari hizo.**

Maoni

Makampuni ya biashara yanaweza kuhusika kwa kusababisha athari kwenye haki za binadamu ama kupitia shughuli zao wenyewe, au kama matokeo ya mahusiano yao ya kibiashara na watu wengine. Kanuni ya 19 ya Mwongozo inafafanua zaidi, juu ya vidokezo vya jinsi makampuni ya biashara yanavyotakiwa kushughulikia hali hii. Kwa madhumuni ya Kanuni hizi za Mwongozo, “shughuli” za kampuni ya biashara zinaelezwa kuwa ni pamoja na vitendo vyote pamoja na vile visivyotekelezwa; na “mahusiano yake ya kibiashara” inaelezwa kuwa ni pamoja na mahusiano na washirika wakibiashara, taasisi katika mzunguko wake wa ongezeko la thamani, na taasisi nyingine yoyote ya mashirika yasiyo ya kiserikali au taasisi za serikali zinazohusiana moja kwa moja na shughuli, bidhaa au huduma zake za biashara.

- 14. Wajibu wa makampuni ya biashara kuheshimu haki za binadamu unahusu makampuni yote bila kujali ukubwa, sekta, mazingira ya uendeshaji, umiliki na muundo wake. Hata hivyo, kipimo na utata wa njia ambazo hutumika kutimiza jukumu hilo zinaweza kutofautiana kutokana na kiwango cha athari kwa haki za binadamu.**

Maoni

Njia ambazo kampuni ya biashara hutumia ili kutimiza wajibu wake wa kuheshimu haki za binadamu zinatakiwa kuwiana na ukubwa wake, pamoja na mambo mengine. Makampuni madogo na yenye ukubwa wa kati yanaweza kuwa na uwezo mdogo na vilevile michakato mingi zaidi isiyo rasmi na miundo ya menejimenti zaidi ya makampuni makubwa, hivyo sera na michakato yao husika itakuwa ya aina tofauti. Hata hivyo makampuni mengine madogo na yenye

ukubwa wa kati yanaweza kusababisha athari mbaya za haki za binadamu, ambazo zitahitaji hatua zinazolingana bila kujali udogo au kubwa wao. Ubaya wa athari utaamuliwa kwa kipimo, upeo na tabia zake zisizorekebishika. Njia ambazo kampuni ya biashara hutumia kutimiza wajibu wake wa kuheshimu haki za binadamu huenda pia zikatofautiana kutegemeana na kama hufanya biashara kupitia kikundi cha kampuni au mtu mmoja mmoja. Hata hivyo, wajibu wa kuheshimu haki za binadamu unayahusu makampuni yote ya biashara kikamilifu na kwa usawa.

15. Ili kukidhi majukumu yao ya kuheshimu haki za binadamu, makampuni ya biashara yanapaswa kuwa na sera na michakato sahihi kwa ukubwa na mazingira yao, ikiwa ni pamoja na:

- (a) Dhamira ya sera kutimiza wajibu wao wa kuheshimu haki za binadamu;**
- (b) Mchakato wa juhudi zinazo stahili kwa haki za binadamu za kutambua, kuzuia, kupunguza na kueleza jinsi wanavyoshughulikia madhara kwa haki za binadamu;**
- (c) Michakato ya kuwezesha urekebishaji wa athari mbaya zozote wanazosababisha au kuchangia kwenye haki za binadamu.**

Maoni

Makampuni ya biashara huhitaji kujua na kuonyesha kwamba yanaheshimu haki za binadamu. Hayawezi kufanya hivyo bila kuwa na sera na taratibu fulani. Kanuni ya 16 hadi 24 zinafafanua zaidi haya.

B. MISINGI YA UTEKELEZAJI JUKUMU LA SERA

16. Msingi wa kuweka wajibu wao wa kuheshimu haki za binadamu, makampuni ya biashara yanapaswa kueleza dhamira yao ya kutimiza jukumu hili kwenye taarifa ya sera ambayo:
- (a) Imeidhinishwa katika ngazi ya juu zaidi ya kampuni hiyo ya biashara;
 - (b) Inafahamika na mtaalamu husika wa ndani na/au nje;
 - (c) Inaeleza matarajio ya wafanyakazi wa kampuni; washirika wa biashara na watu wengine wanaohusiana moja kwa moja na shughuli, bidhaa au huduma zake kwenyehaki za binadamu;
 - (d) Inapatikana kwa umma na kutangazwa ndani na nje kwa wafanyakazi wote, washirika wa biashara na watu wengine wahasika;
 - (e) Inajitokeza katika sera za uendeshaji na taratibu muhimu kwa kuiweka katika taratibu zote za kwenye kampuni yote ya biashara.

Maoni

Neno “taarifa” linatumika kiujumla, kuelezea njia zozote ambazo kampuni hutumia kuelezea majukumu, dhamira, na matarajio yake kwa umma.

Kiwango cha utaalum kinachohitajika ili kuhakikisha kwamba taarifa ya sera inatolewa maelezo ya kutosha kitatofautiana kulingana na ugumu wa shughuli za kampuni. Utaalamu unaweza kuchukuliwa kutoka vyanzo mbalimbali, kama mitandao ya kuaminika au nyenzo za maandishi na hata mashauriano na wataalamu wanaotambulika.

Taarifa ya dhamira lazima ipatikane kwa umma. Ifahamishwe kikamilifu kwa vyombo ambavyo vina mahusiano ya kimkataba na kampuni; wengine wanaohusiana moja kwa moja na shughuli zake, ambao wanaweza kuwa hata na vikosi vya usalama vya Nchi; wawekezaji; na, katika suala la shughuli zenye hatari kubwa kwa haki za binadamu, kwa wadau wenye uwezekano wa kuathirika.

Mawasiliano ya ndani ya taarifa na ya sera na taratibu zinazohusiana yanapaswa kuweka wazi mipaka na mifumo ya uwajibikaji utakavyofanyika, na ziungwe mkono na mafunzo yoyote muhimu kwa ajili ya wafanyakazi katika kazi husika za biashara.

Kama Nchi zinavyopaswa kufanya kazi ya kupata sera inayoeleweka, inabidi na makampuni yajitahidi kuoanisha kati ya wajibu wao wa kuheshimu haki za binadamu na sera na taratibu zinazoongoza shughuli na mahusiano yao ya biasharakwa upana. Hii ni pamoja na, kwa mfano, sera na taratibu ambazohupanga fedha na motisha nyingine za kiutendaji kwa ajili ya wafanyakazi; taratibu za manunuzi; na shughuli za ushawishi pale ambapo haki za binadamu zipo hatarini kuvunjwa.

Kwa njia hizi na nyingine zozote zinazofaa, taarifa ya sera lazima iainishe kuanzia ngazi ya juu ya kampuni ya biashara kupitia kazi zake zote, ambazo vinginevyo zinaweza kutenda bila kufahamu au kujali haki za binadamu.

JUHUDI ZA HAKI ZA BINADAMU ZINAZOSTAHILI

17. Ili kubaini, kuzuia, kupunguza na kuelezea jinsi wanavyo shughulikia athari mbaya kwa haki za binadamu, makampuni ya biashara yanapaswa kufanya juhudi zinazostahili kulinda haki za binadamu. Mchakato huo lazima uwe pamoja na kutathmini athari kwa haki za binadamu halisi na zenye uwezekano wa kutokea, kuingiza na kushughulikia matokeo ya utafiti, kufuatilia majibu, na kufahamisha jinsi athari zinavyoshughulikiwa. Juhudi za haki za binadamu zinazostahili:
- (a) Zishughulikie athari mbaya kwa haki za binadamu ambazo kampuni ya biashara inaweza kusababisha au kuchangia kusababisha kupitia shughuli zake yenyewe, au ambayo inaweza kuhusiana moja kwa moja na shughuli, bidhaa au huduma zake kwa mahusiano yake ya kibiashara;
 - (b) Athari hizi zitatofautiana katika ugumu na ukubwa wa kampuni ya biashara, mazingira ya uwezekano wa kusababisha athari kwa haki za binadamu, na aina na mazingira ya shughuli zake;
 - (c) Ziwe endelevu, zinazotambua kwamba hatari kwa haki za binadamu zinaweza kubadilika kadiri shughuli za kampuni ya biashara na mazingira ya uendeshaji yanapopanuka.

Maoni

Kanuni hii inafafanua vigezo vya juhudi kwa haki za binadamu zinazostahili, wakati Kanuni ya 18 kupitia kanuni ya 21 inafafanua vipengele vyake muhimu.

Hatari kwa haki za binadamu zinaeleweka kuwa athari mbaya kwa haki za binadamu, zenye uwezekano wa kutokea kulingana na shughuli za kampuni ya biashara. Athari zenye uwezekano zinapaswa zishughulikiwe kwa kuzuia au kuzipunguza, wakati athari halisi, yaani zile ambazo tayari zimeshatokea, zinapaswa kupatiwa ufumbuzi (Kanuni ya 22).

Juhudi zinazostahili, kwa haki za binadamu, zinaweza kujumuishwa katika mifumo mipana ya usimamizi wa athari zinazosababishwa na kampuni, ili mradi iwe zaidi ya kutambua na kusimamia hatari za vitu kwa kampuni yenyewe, kujumuisha na hatari kwa haki za wamiliki. Juhudi kwa haki za binadamu zinastahili zianzishwe mapema iwezekanavyo katika kuendeleza shughuli au uhusiano mpya, kutokana na kwamba hatari kwa haki za binadamu zinaweza kuwa zimeshaongezeka au kupunguzwa wakati wa kuunda mikataba au makubaliano mengine, na zinaweza kurithiwa kupitia muunganiko au ununuzi.

Pale ambapo makampuni ya biashara yana idadi kubwa ya vyombo katika mzunguko wao wa thamani inaweza kuwa vigumu kufanya juhudi zinazostahili kukabiliana na athari zote mbaya kwa haki za binadamu. Kama ni hivyo, makampuni ya biashara lazima yatambue maeneo ya jumla ambapo hatari ya athari mbaya kwa haki za binadamu ni kubwa zaidi, iwe kutokana na mazingira ya uendeshaji wa baadhi ya wauzaji au wateja, shughuli fulani, bidhaa au huduma zinazohusika, au mambo mengine yanayohusika, na kutoa kipaumbele kwa juhudi stahiki kwa haki za binadamu.

Masuala ya ushiriki yanaweza kutokea wakati kampuni ya biashara inapochangia, au inapoonekana kuwa inachangia na kusababisha athari

mbaya kwa haki za binadamu zinazosababishwa na watu wengine. Ushiriki una maana zisizo za kisheria, hali kadhalika na za kisheria. Kama suala lisilo la kisheria, makampuni ya biashara yanaweza kuonekana “mshiriki” katika matendo ya upande mwingine ambapo, kwa mfano, yanaonekana kunufaika na ukiukwaji unaofanywa na watu wengine.

Kama suala la kisheria, mamlaka za kisheria nyingi za kitaifa hupiga marufuku kushiriki katika kufanya uhalifu. Mamlaka nyingi huyawajibisha kisheria makampuni ya biashara katika makosa ya jinai kwenye masuala hayo. Kwa kawaida, vitendo ya raia/mtu pia vinaweza kutegemea mchango wa madhara yanayodaiwa kufanywa na kampuni, ingawa haya yanaweza yasielezewe katika masharti ya haki za binadamu. Uzito wa falsafa ya sheria ya kimataifa ya makosa ya jinai unaonyesha kuwa kiwango husika kwa ajili ya kusaidia nakushawishi vitendo au uhamasishaji wenye athari kubwa kwa vitendo vya kihalifu.

Kufanya juhudi sahihi zinazostahili za haki za binadamu lazima kusaidie makampuni ya biashara kushughulikia madai ya kisheria dhidi yao kwa kuonyesha kwamba walichukua kila hatua iliyofaa kuepuka kujihusisha na ukiukwaji wa haki za binadamu wanaodaiwa kuufanya. Hata hivyo, makampuni ya biashara yanayofanya juhudi hizo yasichukulie kwamba, hii yenyewe, itawaepusha kabisa au moja kwa moja na uwajibikaji wa kusababisha au kuchangia katika ukiukwaji wa haki za binadamu.

- 18. Ili kupima hatari kwa haki za binadamu, makampuni ya biashara yanapaswa kutambua na kutathmini athari zote mbaya kwa haki za binadamu, zilizo halisi au zenye**

uwezekano wa kutokea na ambazo zinaweza kuhusika, ama kupitia shughuli zao wenyewe au kama matokeo ya mahusiano yao ya kibiashara. Mchakato huu unapaswa:

- (a) Kutumia utaalum wa haki za binadamu wa ndani na/au wa kujitegemea wa nje;**
- (b) Kushirikisha ushauri muhimu na makundi yenye uwezekano wa kuathirika na wadau wengine muhimu, kulingana na ukubwa wa kampuni ya biashara na aina na mazingira ya shughuli hiyo.**

Maoni

Hatua ya awali katika kufanya juhudi zinazostahili za haki za binadamu ni kutambua na kutathmini aina ya athari mbaya za haki za binadamu, zilizo halisi na zile zenye uwezekano wa kuwepo, ambazo kampuni ya biashara inaweza kuhusika. Madhumuni yake ni kuelewa athari maalum kwa watu maalum, kutokana na mazingira maalum ya shughuli. Kwa kawaida hii ni pamoja na kutathmini mazingira ya haki za binadamu kabla ya mapendekezo ya shughuli ya biashara, pale inapowezekana; kutambua nani anaweza kuathirika; kuorodhesha viwango na masuala husika ya haki za binadamu; na kuonyesha jinsi shughuli zilizopendekezwa na mahusiano yanayohusishwa na biashara yanavyoweza kuwa na athari mbaya kwa haki za binadamu kwa wale waliotajwa.

Katika mchakato huu, makampuni ya biashara yanapaswa kuchukua tahadhari maalum kwa athari zozote kwa haki za binadamu kwa watu kutoka vikundi au jamii ambayo inaweza kuwa katika hatari kubwa ya mazingira magumu au kutengwa, na kuzingatia hatari mbalimbali zinazoweza kuwakabili wanawake na wanaume.

Mchakato wa kutathmini athari kwa haki za binadamu inaweza kuwekwa katika mchakato mingine kama vile tathmini ya hatari au tathmini ya athari za kimazingira na kijamii, zinapaswa zijumuishe haki za binadamu zote zinazotambuliwa kimataifa kama rejea, kwa kuwa makampuni ya biashara yanaweza kuathiri haki zozote kati ya hizo.

Kwa kuwa hali ya haki za binadamu hubadilika, tathmini ya athari kwa haki za binadamu lazima zifanywe mara kwa mara: kabla ya shughuli au uhusiano mpya; kabla ya uamuzi au mabadiliko muhimu katika operesheni (kwa mfano kuingia katika soko, uzinduzi wa bidhaa, mabadiliko ya sera, au mabadiliko makubwa kwa biashara); katika kukabiliana au matarajio ya mabadiliko katika mazingira ya uendeshaji (kwa mfano kuleta mvutano wa kijamii); na mara kwa mara katika kipindi chote cha shughuli au uhusiano.

Ili kuyawezesha makampuni ya biashara kutathmini athari kwa haki za binadamu kwa usahihi, yanapaswa kufanya bidii ya kuelewa matatizo ya wadau wenye uwezekano wa kuathirika kwa kupata ushauri kutoka kwao moja kwa moja katika njia inayozingatia lugha na vikwazo vingine vyenye uwezekano wa kutokea kwa ushiriki wenye ufanisi. Katika hali ambapo ushauri huo hauwezekani, makampuni ya biashara lazima yafikirie njia mbadala ya kuridhisha kama vile kuwasiliana na wataalam wa kuaminika, wanaojitegemea, ikiwa ni pamoja na watetezi wa haki za binadamu na wengine kutoka asasi za kiraia.

Tathmini ya athari kwa haki za binadamu hutoa taarifa za hatua zinazofuata katika mchakato wa juhudi kwa haki za binadamu.

Tathmini ya athari za haki za binadamu hutoa taarifa za hatua zinazofuata katika mchakato wa juhudi za haki za binadamu.

19. Ili kuzuia na kupunguza athari mbaya kwa haki za binadamu, makampuni ya kibiashara lazima yahusishe matokeo ya tathmini zao za athari katika kazi na michakato husika ya ndani pamoja na taratibu ili kuchukua hatua sahihi.

(a) Ushirikiano wenye ufanisi unahitaji:

- (i) Wajibu wa kushughulikia madhara kama hayo upewe kwa watu wenye ngazi fulani na kazi inayofaa ndani ya mampuni ya kibiashara;**
- (ii) Michakato ya ufanyaji maamuzi ya ndani, mgao wa bajeti na usimamizi iwawezeshe katika kukabiliana kikamilifu na athari hizo.**

(b) Hatua sahihi zitatofautiana kulingana na:

- (i) Kama kampuni ya biashara imesababisha au kuchangia athari mbaya, au kama inahusishwa tu moja kwa moja na shughuli, bidhaa au huduma zake kwa uhusiano wa kibiashara;**
- (ii) Kiwango cha uwezo wake katika kushughulikia athari hizo mbaya**

Maoni

Ushirikiano katika kampuni ya biashara wa matokeo maalum utawezekana tu kama kutathmini athari kwa haki za Binadamu, kunaweza kuwa kwa ufanisi iwapo tu dhamira yake ya kisera ya haki za binadamu imeingizwa katika kazi zote za biashara husika. Hii inahitajika ili kuhakikisha kwamba matokeo ya tathmini yanaeleweka vizuri na yanapewa uzito unaostahili na kuchukuliwa hatua.

Katika kutathmini athari kwa haki za binadamu, makampuni ya biashara yatakuwa yameangalia athari mbaya pia zile zinazoweza kutokea. Athari zenye uwezekano wa kutokea lazima zizuiliwe au kupunguzwa kwa njia ya ushirikiano wa usawa wa matokeo kwa makampuni yote ya biashara. (Kanuni ya 22).Pale ambapo kampuni ya biashara husababisha au inaweza kusababisha athari mbaya kwa haki za binadamu, ni lazima hatua muhimu zichukuliwe kusitisha au kuzuia athari hiyo.

Pale ambapo kampuni ya biashara inachangia au inaweza kuchangia athari mbaya kwa haki za binadamu, ni lazima kuchukua hatua muhimu ili kusitisha au kuzuia mchango wake na kutumia uwezo wake kupunguza athari yoyote iliyobaki kwa kiasi kikubwa iwezekanavyo. Uwezo unachukuliwa kuwepo pale ambapo kampuni ina uwezo wa kuleta mabadiliko katika utendaji mbaya wa chombo kinachosababisha madhara.

Pale ambapo kampuni ya biashara haikuchangia kuleta athari mbaya kwa haki za binadamu, lakini hata hivyo athari hiyo haihusishwi moja kwa moja na shughuli, bidhaa au huduma zake kwa uhusiano wa biashara yake na chombo kingine, hali huwa ngumu zaidi. Kati ya sababu ambazo zitaamua hatua sahihi zakuchukuliwa katika hali kama hiyo ni uwezo wa kampuni hiyo kwa chombo kinachohusika, umuhimu wa uhusiano huo kwa kampuni, ukubwa wa ukiukwaji, na iwapo kuvunja uhusiano na chombo chenyewe kungekuwa na matokeo mabaya kwa haki za binadamu

Kadri hali na athari zake kwa haki za binadamu zinavyokuwa na ugumu, ndivyo kadri suala hili linavyokuwa na nguvu zaidi kwa kampuni ya biashara kutumia ushauri wa wataalam wa kujitegemea katika kuamua jinsi ya kulishughulikia.

Kama kampuni ya biashara ina uwezo wa kuzuia au kupunguza athari mbaya, inabidi itumie uwezo huo. Kama haina uwezo kunaweza kuwa na njia za kampuni za kuongeza uwezo kwa mfano, kwa kujenga uwezo au kutoa motisha nyingine kwa chombo husika, au kushirikiana na wadau wengine.

Kuna hali ambazo kampuni hukosa uwezo wa kuzuia au kupunguza athari mbaya na haiwezi kuongeza uwezo wake. Ikiwa katika hatua hii, kampuni inapaswa kufikiria kukomesha uhusiano huo kwa kuzingatia tathmini za kuaminika za athari mbaya kwa haki za binadamu zenye uwezekano kufanya hivyo.

Pale ambapo uhusiano ni “muhimu” kwa kampuni, kuvunja huleta changamoto. Uhusiano unaweza kuonekana kuwa muhimu kama unatoa bidhaa au huduma ambayo ni muhimu kwa kampuni ya biashara, na ambayo haina chanzo mbadala. Hapa ukubwa wa athari mbaya kwa haki za binadamu lazima pia uzingatiwe: Kadri ukiukwaji unavyokuwa mkubwa ndivyo kadri kampuni itakavyohitaji kuona mabadiliko ya haraka zaidi kabla haijachukua uamuzi iwapo inabidi ivunje uhusiano au la. Kwa kuwa ukiukwaji unaendelea na kampuni bado ipo katika uhusiano huo inapaswa kuonyesha jitihada zake yenyewe zinazoendelea za kupunguza athari hiyo na kuwa tayari kukubali matokeo yoyote ya sifa kifedha au kisheria ya uhusiano unaoendelea.

- 20. Ili kuthibitisha kama athari mbaya kwa haki za binadamu zinapatiwa ufumbuzi, makampuni ya biashara yanapaswa kufuatilia ufanisi wa hatua zao. Ufuatiliaji unatakiwa:**
(a) Kuzingatia viashiria sahihi vya kimaelezo na kitarakimu;

- (b) Kutumia maoni kutoka vyanzo vya ndani na vya nje,**
- (c) ikiwa ni pamoja na ya wadau walioathirika.**

Maoni

Ufuatiliaji ni muhimu kwa kampuni ya biashara kujua kama sera zake za haki za binadamu zinatekelezwa ipasavyo pia kama imeshughulikia vizuri athari kwa haki za binadamu zilizotajwa na kuchochea uendelevu wa uboreshaji wake.

Makampuni ya biashara yanapaswa kufanya juhudi maalum kufuatilia ufanisi wa hatua zao walizochukua kwa athari za watu binafsi, kutoka vikundi au watu wanaoweza kuwa katika hatari kubwa ya mazingira magumu au kutengwa.

Ufuatiliaji unapaswa kujumuishwa katika michakato husika ya ndani ya kutoa taarifa.

Makampuni ya biashara yanaweza kutumia zana ambazo tayari hutumika katika masuala mengine. Hii inaweza kuwa pamoja na mikataba ya utendaji na uhakiki, vile vile tafiti na ukaguzi. Pia kwa kutumia taarifa zilizogawanya jinsia pale ilipofaa. Taratibu za malalamiko za ngazi ya uendeshaji zinaweza pia kutoa maoni muhimu juu ya ufanisi wa juhudi zinazostahili za makampuni ya biashara kwa haki za binadamu kutoka kwa wale walioathirika moja kwa moja. (Tazama Kanuni ya 29).

- 21. Ili kueleza jinsi wanavyoshughulikia athari zao kwa haki za binadamu, makampuni ya biashara yanapaswa kuwa tayari kutoa taarifa hizo nje, hasa matatizo yanapotolewa na wadau walioathirika au kwa niaba yao. Makampuni ya**

biashara ambayo shughuli zao au mazingira ya uendeshaji yanasababisha hatari za athari kubwa kwa haki za binadamu, zinapaswa kutoa taarifa rasmi juu ya namna wanavyokabiliana nayo. Katika matukio yote mawasiliano yanatakiwa:

- (a) Kuwa ya aina na marudio yanayoonyesha athari za kampuni ya biashara kwa haki za binadamu na kwamba yanapatikana kwa hadhira iliyokusudiwa;**
- (b) Kutoa taarifa ambazo zinatoshleza kufanya tathmini ya utoshelevu wa hatua iliyochukuliwa na kampuni kwa athari maalum kwa haki za binadamu, iliyohusika;**
- (c) Kwa upande wake kutohatarisha wadau walioathirika, wafanyakazi au kwa mahitaji halali ya usiri wa kibiashara.**

Maoni

Wajibu wa kuheshimu haki za binadamu unahitaji makampuni ya biashara yawe na sera na michakato ambayo wanaweza kujua na kuonyesha kwamba wanaheshimu haki za binadamu katika utendaji wake. Kuonyesha kunahusisha mawasiliano, kutoa kiwango cha uwazi na uwajibikaji kwa watu binafsi au vikundi ambavyo vinaweza kuwa vimeathiriwa na kwa wadau wengine muhimu, ikiwa ni pamoja na wawekezaji.

Mawasiliano yanaweza kuwa ya aina mbalimbali, ikiwa ni pamoja na mikutano ya ana kwa ana, majadiliano katika mtandao, kushauriana na wadau walioathirika, na taarifa rasmi kwa umma. Utoaji rasmi wa taarifa wenyewe umekuwa, kutoka taarifa ya jadi ya kila mwaka na taarifa za uwajibikaji/endelevu wa makampuni, zikijumuisha taarifa mpya katika mtandao na taarifa jumuishi za fedha na zisizo za kifedha.

Utoaji rasmi wa taarifa wa makampuni ya biashara unatarajiwa ufanyike pale ambapo pana hatari za athari kubwa za binadamu, iwe ni kutokana na aina ya shughuli ya biashara au mazingira ya uendeshaji. Taarifa lazima iwe na mada na viashiria kuhusu jinsi makampuni yanavyotambua na kushughulikia athari mbaya kwa haki za binadamu. Uthibitishaji wa kujitegemea wa utoaji taarifa za haki za binadamu unaweza kuimarisha maudhui na kuaminika kwake. Viashiria maalum vya sekta vinaweza kutoa maelezo ya ziada yenye manufaa.

UREKEBISHAJI

22. Pale makampuni ya biashara yanapotambua kuwa yamesababisha au kuchangia athari mbaya yanapaswa kusaidia au kushirikiana katika urekebishaji wake kupitia michakato halali.

Maoni

Hata pamoja na sera na utendaji bora, kampuni ya biashara inaweza kusababisha au kuchangia athari mbaya kwa haki za binadamu ambayo haikutabiri au kuweza kuzuia.

Pale ambapo kampuni ya biashara inatambua hali hiyo iwe ni kupitia mchakato wake wa juhudi zinazostahili za haki za binadamu au njia nyingine. Wajibu wake wa kuheshimu haki za binadamu unahitaji ushiriki kamili katika urekebishaji au kwa kushirikiana na watendaji wengine. Taratibu za malalamiko za ngazi ya uendeshaji kwa wale wenye uwezekano wa kuathiriwa na shughuli za kampuni ya biashara inaweza kuwa moja ya njia bora za kuwezesha urekebishaji wanapotimiza vigezo fulani muhimu, kama inavyoelezwa katika Kanuni ya 31.

Pale ambapo imetokea kwamba kampuni ya biashara haikusababisha au kuchangia athari mbaya lakini inahusishwa moja kwa moja na shughuli na bidhaa au huduma zake kwa uhusiano wa kibiashara. Wajibu wa kuheshimu haki za binadamu hauhitaji kampuni isaidie katika urekebishaji ingawa inaweza kufanya hivyo.

Hali nyingine, hasa pale ambapo inadaiwa kufanyika kwa uhalifu wa kawaida kampuni itahitajika kushirikiana na taratibu za kisheria.

Mwongozo zaidi juu ya taratibu ambazo urekebishaji unaweza kufanywa, ikiwa ni pamoja na kupingwa kwa madai ya athari mbaya kwa haki za binadamu, yamo katika sura ya III katika upatikanaji wa urekebishaji.

MASUALA YA KIMUKTADHA

- 23. Makampuni ya biashara katika kila muktadha yanatakiwa:**
- (a) Kuzingatia sheria zote husika na kuheshimu haki za binadamu zinazotambuliwa kimataifa popote pale wanapofanya kazi;**
 - (b) Kutafuta njia za kuheshimu kanuni za haki za binadamu zinazotambuliwa Kimataifa wanapokabiliwa na mahitaji ya kutatanisha;**
 - (c) Kushughulikia hatari ya kusababisha au kuchangia ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu na ukiukwaji wa kisheria popote pale wanapofanya kazi.**

Maoni

Ingawa kila nchi na muktadha wake wa ndani unaweza kuathiri haki za binadamu na shughuli za biashara na mahusiano ya kibiashara

makampuni ya biashara yote yana wajibu huo wa kuheshimu haki za binadamu popote wanapofanya kazi. Pale ambapo mazingira ya ndani yanaonekana kutowezekana kutimiza wajibu huu kikamilifu, makampuni ya biashara yanatarajiwa kuheshimu kanuni za haki za binadamu zinazotambuliwa kimataifa kwa kiasi kikubwa iwezekanavyo katika mazingira hayo na kuweza kuonyesha jitihada zao katika suala hili.

Baadhi ya mazingira ya uendeshaji kama vile maeneo yaliyoathirika na vita yanaweza kuongeza hatari ya makampuni kuwa na makosa katika ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu unaofanywa na watendaji wengine (vikosi vya usalama, kwa mfano). Makampuni ya biashara yashughulikie hatari hii kama suala la kuzingatiwa kisheria kutokana na kupanuka kwa mtandao wa uwezo wa kampuni na dhima ya kisheria kutokana na madai ya raia nje ya sheria za nchi na kutaka kuingizwa kwa masharti ya Katiba ya Mahakama ya Kimataifa ya Jinai katika mamlaka za kisheria yanayotoa jukumu la jinai kwa kampuni. Aidha, wakurugenzi wa makampuni, maafisa na wafanyakazi wanaweza kuwa chini ya dhima ya binafsi kwa vitendo ambavyo vimefikia ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu.

Katika mazingira tata kama haya, makampuni ya biashara yanapaswa kuhakikisha kuwa hayafanyi hali hiyo kuwa mbaya zaidi. Katika kutathmini namna bora ya kushughulikia, mara nyingi watahuriwa kutotumia utaalumu na mashauriano na wataalam mbalimbali wa ndani ya kampuni tu, bali pia kushauriana na wataalam wa kujitegemea na wa kuaminika nje ya kampuni zikiwemo Serikali, asasi za kiraia, taasisi za haki za binadamu kitaifa na mipango husika ya wadau mbalimbali.

- 24. Ikibidi kuzipa kipaumbele hatua za kushughulikia athari mbaya kwa haki za binadamu zinazo weza kutokea au zilizo halisi. Makampuni ya biashara lazima kwanza yajitahidi kuzuia na kupunguza athari mbaya zaidi au pale ambapo kuchelewa kuchukua hatua hufanya athari hizo zisiweze kurekebisha.**

Maoni

Wakati makampuni ya biashara yanapaswa kushughulikia athari zao mbaya zote kwa haki za binadamu haitawezekana siku zote kuzishughulikia kwa wakati mmoja. Pale pasipo na mwongozo maalum wa kisheria makampuni ya biashara yaanze na zile athari kwa haki za binadamu zitakazokuwa mbaya zaidi, kwa kutambua kwamba ucheleweshwaji wa kuchukua hatua unaweza kuathiri urekebishaji wa hali. Ubaya si dhana kamili katika mukhtadha huu bali una uhusiano na athari nyingine kwa haki za binadamu ambazo kampuni hiyo ya biashara imebainisha.

SURA YA TATU

III. UFIKIWAJI WA MAREKEBISHO

A. KANUNI ZA MSINGI

- 25. Kama sehemu ya wajibu wao wa kulinda haki za binadamu zinazohusiana na biashara zisikiukwe, Nchi lazima zichukue hatua zinazofaa ili kuhakikisha, kwa kupitia njia ya mahakama, kiutawala, kisheria au njia nyingine sahihi, kwamba wakati ukiukwaji huo unapotokea ndani ya nchi yao na/au mamlaka ya kisheria wale walioathirika wanapatiwa ufumbuzi unaofaa.**

Maoni

Bila kuchukua hatua muafaka za kuchunguza, kukemea na kurekebisha ukiukwaji wa haki za binadamu unaohusiana na biashara unapotokea, wajibu wa Nchi kulinda unaweza kufanywa dhaidu au kutokuwa na maana.

Upatikanaji wa ufumbuzi wa kufaa una vipengele vya kiutaratibu na vile vya kivitendo. Ufumbuzi unaotolewa na taratibu za kushughulikia malalamiko zilizojadiliwa katika sehemu hii unaweza kuwa katika aina mbalimbali za vitendo, lengo ambalo kwa ujumla, litakuwa kuzuia na/ au kurekebisha madhara yoyote kwa haki za binadamu yaliyotokea. Marekebisho yanaweza kuwa kuomba msamaha, kufanya malipo, urekebishaji, fidia ya kifedha au isiyo ya kifedha na kuidhinisha adhabu (inaweza kuwa ya jinai au ya kiutawala, kama vile faini), na

vile vile kuzuia madhara, kwa mfano kwa njia ya amri ya mahakama au dhamana zisizorudiwa.

Taratibu za kutoa ufumbuzi zisiwe na upendeleo, zilindwe dhidi ya rushwa na zisipate vishawishi vya kisiasa au mengine yoyote ya kushawishi matokeo.

Kwa madhumuni ya Kanuni hizi za Mwongozo, malalamiko yanaeleweka kuwa dhuluma iliyobainika na kuamsha hisia za haki za mtu binafsi au kikundi, zenye misingi ya sheria, mkataba, ahadi iliyo bayana au zisizotajwa bayana, mila, au fikra za ujumla za usawa kwa jamii kutoridhishwa na hali. Istilahi utaratibu wa kushughulikia malalamiko/kero hutumika kuonyesha mchakato wowote wa Serikali au usio wa Serikali, wa kimahakama au usio wa kimahakama, uliowekewa utaratibu, ambao malalamiko juu ya ukiukwaji wa haki za binadamu unaohusiana na biashara yanaweza kutolewa na ufumbuzi ukatafutwa.

Taratibu za nchi za kushughulikia malalamiko/kero zinaweza kusimamiwa na tawi au wakala wa Nchi, au na chombo cha kujitegemea kisheria au kikatiba, zinaweza kuwa za kimahakama au zisizo za kimahakama. Katika baadhi ya taratibu, wale walioathirika na ukiukwaji hushirikishwa moja kwa moja katika kutafuta utatuzi; nyingine, msuluhishi hutafuta ufumbuzi kwa niaba yao. Mifano hii ni pamoja na mahakama (kwa hatua za makosa ya jinai na vile vile ya mada), mahakama za kazi, taasisi za haki za binadamu za kitaifa, Vituo vya Mawasiliano vya Taifa chini ya Miongozo ya Makampuni ya kimataifa ya Shirika la Ushirikiano na Maendeleo ya Kiuchumi, ofisi nyingi za wachunguzi wa malalamiko, na ofisi za malalamiko zinazoendeshwa na Serikali.

Kuhakikisha upatikanaji wa ufumbuzi kwa ukiukwaji wa haki za binadamu unaohusiana na biashara kunahitaji pia Nchi ziwezeshe uelewa wa umma na uelewa wa taratibu hizi, jinsi zinavyoweza kupatikana, na msaada wowote (wa fedha au mtaalam) wa kufanya hivyo.

Taratibu za kimahakama na zisizokuwa za kimahakama za kushughulikia malalamiko zinapaswa kuunda aina ya msingi wa mfumo mpana wa utatuzi. Ndani ya mfumo huo, taratibu za kushughulikia malalamiko za ngazi ya uendesaji zinaweza kutoa njia za kupata msaada na suluhisho mapema. Taratibu za kushughulikia malalamiko za ngazi ya uendesaji, kwa upande wake, zinaweza kuongezwa au kuimarishwa kwa ushirikiano wa kazi za urekebishaji na pia taratibu za haki za binadamu kimataifa na kikanda. Mwongozo zaidi kuhusiana na taratibu hizi zinatolewa katika Kanuni za Mwongozo za 26 hadi 31.

B. KANUNI ZA UENDESHAJI

TARATIBU ZA KIMAHAKAMA ZA NCHI

26. Nchi zinapaswa kuchukua hatua zinazofaa ili kuhakikisha ufanisi wa taratibu za ndani za mahakama zinaposhughulikia ukiukwaji wa haki za binadamu zinazohusiana na biashara, zikiwemo kuzingatia njia za kupunguza vikwazo vya kisheria, vitendo na vikwazo vingine husika vinavyoweza kusababisha kunyimwa kwa utatuzi.

Maoni

Taratibu za mahakama zenye ufanisi ni sehemu muhimu sana ya kuhakikisha upatikanaji wa suluhisho.

Uwezo wao wa kushughulikia ukiukwaji wa haki za binadamu zinazohusiana na biashara hutegemea uadilifu, uaminifu na uwezo wao wa kufuata mchakato stahiki.

Nchi zinapaswa kuhakikisha kwamba haziweki vikwazo vya kuzuia kesi halali kufikishwa mbele ya mahakama katika hali ambapo mchakato wa mahakama ni sehemu muhimu ya kupata ufumbuzi au vyanzo mbadala vya utatuzi wa kufaa pale ambapo ufumbuzi wa kufaa haupatikani. Zinapaswa pia kuhakikisha kwamba utoaji haki hauzuiliwi kwa rushwa kwenye taratibu za kimahakama, kwamba mahakama hazipati shinikizo la kiuchumi au kisiasa kutoka kwa mawakala wa Nchi nyingine na kutoka kwa watendaji wa biashara, na kwamba shughuli halali na za amani za watetezi wa haki za binadamu haziwekewi vipingamizi.

Vikwazo vya kisheria ambavyo vinaweza kuzuia kesi halali zinazohusisha ukiukwaji wa haki za binadamu unaohusiana na biashara-zisishughulikiwe vinaweza kutokea pale ambapo, kwa mfano:

- Njia ambayo wajibu wa kisheria unaohusisha wanakikundi wa makampuni chini ya sheria ya ndani ya nchi ya makosa ya jinai na ya madai huepusha uwajibikaji sahihi;
- Pale ambapo wadai wananyimwa haki katika Nchi mwenyeji na hawawezi kufika katika mahakama ya Nchi walipotokea bila kujali uhalali wa madai hayo;
- Pale ambapo makundi fulani, kama vile wazawa na wahamiaji,

wanatengwa kupata ulinzi sawa wa kisheria wa haki za binadamu ambao ni wa watu wote.

Vikwazo vya vitendo na kiutaratibu vya kupata utatuzi wa kimahakama vinaweza kutokea pale ambapo, kwa mfano:

- Gharama za kupeleka madai ni kubwa mno kiasi cha kufaa kuwa kipingamizi sahihi kwa kesi zisizostahili na/au haziwezi kupunguzwa kwa viwango vya kuridhisha kupitia msaada wa serikali, taratibu “za soko” (kama vile madai ya miundo ya bima na ada za kisheria zinazohusu kesi), au kwa njia nyingine;
- Wadai hupata matatizo katika kupata uwakilishi wa kisheria, kutokana na ukosefu wa rasilimali au motisha nyingine kwa ajili ya kuwapa wanasheria ili wawashauri wadai katika eneo hili;
- Kuna uhaba wa taratibu kwa madai mchanganyiko au kuwezesha mashauri ya uwakilishi (kama vile hatua za tabaka fulani na taratibu nyingine za hatua za pamoja), na hii huzuia ufumbuzi wa kufaa kwa wadai binafsi;
- Waendesha mashitaka hawana rasilimali, utaalamu na msaada wa kutosha kwa ajili ya kutimiza majukumu ya Nchi zao ya kuchunguza ushiriki wa watu binafsi na biashara katika uhalifu unaohusiana na haki za binadamu.

Wingi wa vikwazo hivi ni matokeo ya/ au vimezungukwa na, kukosekana kwa usawa mara kwa mara kati ya pande husika kwa madai ya haki za binadamu zinazohusiana na biashara. Huu ni usawa kama vile katika rasilimali zao za fedha, upatikanaji wa habari na utaalamu. Aidha, iwe ni kwa ubaguzi wa wazi au kama matokeo yasiyotarajiwa, ya jinsi mifumo ya mahakama inavyoundwa na kufanya kazi, watu binafsi kutoka vikundi au watu walio katika hatari

kubwa ya kuwa katika mazingira magumu au kutengwa mara nyingi hukabiliwa na vipingamizi vya ziada kitamaduni, kijamii, kimwili na kifedha vya kupata, kutumia na kunufaika na taratibu hizi. Uzingativu maalum uwekwe katika haki na mahitaji maalum ya makundi au watu hao katika kila hatua ya mchakato wa kutafuta ufumbuzi: upatikanaji, taratibu na matokeo.

TARATIBU ZA NCHI ZA KUSHUGHULIKIA MALALAMIKO YASIYO YA KIMAHAKAMA

- 27. Serikali za Nchi husika zinapaswa kutoa taratibu za kushughulikia malalamiko yasiyokuwa ya kimahakama yanayofaa na sahihi, sambamba na taratibu za mahakama, kama sehemu ya mfumo wa Nchi unao eleweka kwa ajili ya kupatiwa ufumbuzi wa ukiukwaji wa haki za binadamu unaohusiana na biashara.**

Maoni

Utawala, sheria na taratibu nyingine zisizokuwa za kimahakama hutekeleza jukumu muhimu katika kukamilisha na kuboresha taratibu za mahakama. Hata pale ambapo mifumo ya mahakama ni ya ufanisi na yenye nyenzo za kutosha, haziwezi kubeba mzigo wa kushughulikia madai ya kila ukiukwaji. Utatuzi wa mahakama hauhitajiki wakati wote; na wala si njia inayopendelewa kwa wadai wote. Mapungufu katika utoaji ufumbuzi wa ukiukwaji wa haki za binadamu yanayohusiana na biashara yanaweza kurekebisha, pale inapofaa, kwa kupanua wigo wa mamlaka ya taratibu zilizopo zisizokuwa za kimahakama na/au kwa kuongeza taratibu mpya. Taratibu hizi zinaweza kuwa za upatanishi, uamuzi rasmi au kufuata michakato mingine mwafaka kitamaduni na haki linganifu - au kuhusisha taratibu mbalimbali hizi kutegemeana na masuala husika. Maslahi yoyote ya umma yanayohusika, na mahitaji

ya pande hizo yanayowezekana kuwepo. Ili kuhakikisha ufanisi wao, zinapaswa kutekeleza vigezo vilivyowekwa katika Kanuni ya 31.

Taasisi za kitaifa za haki za binadamu zina jukumu muhimu la kutekeleza suala hili.

Kama ilivyo kwa mifumo ya mahakama, Nchi zinapaswa kufikiria njia ya kushughulikia ukosefu wa usawa wowote kati ya pande hizi na madai ya haki za binadamu yanayohusiana na biashara na vikwazo vyovyote vya ziada vilivyopo vinavyowakabili watu binafsi kutoka vikundi au jamii walio katika hatari kubwa ya mazingira magumu au waliobaguliwa.

TARATIBU ZISIZO ZA KISERIKALI ZA KUSHUGHULIKIA MALALAMIKO

28. Nchi zinapaswa kuweka mipago ya kuwezesha upatikanaji wa njia zisizo za kiserikali zinazofaa za kushughulikia madhara kwa haki za binadamu yatokanayo na biashara.

Maoni

Upande mmoja wa taratibu zisizo za kiserikali zinazofaakushughulikia malalamiko zinawahusu wale wanaosimamiwa na kampuni ya biashara peke yake au na wadau, kwa muungano wa viwanda au kikundi cha wadau mbalimbali. Taratibu hizo si za kimahakama, lakini zinaweza kutumia uamuzi, taratibu za mazungumzo au taratibu nyingine mwafaka na haki linganifu. Taratibu hizi zinaweza kuwa na manufaa fulani kama vile upatikanaji wa ufumbuji wa haraka, kupunguza gharama na/au kufikia mataifa mbalimbali.

Upande mwingine unajumuisha vyombo vya haki za binadamu vya kikanda na kimataifa. Hivi mara nyingi vimeshughulikia madai ya Nchi kukiuka majukumu yake ya kuheshimu haki za binadamu. Hata hivyo, vingine vimeshughulikia pia na kushindwa kwa serikali kutimiza wajibu wake wa kulinda ukiukwaji wa haki za binadamu unaofanywa na makampuni ya biashara.

Nchi zinaweza kutekeleza jukumu la kuongeza uelewa, au kuwezesha upatikanaji wa, taratibu mbadala, sambamba na taratibu zinazotolewa na Nchi yenyewe.

29. Ili kufanya malalamiko yaweze kushughulikiwa mapema na kupatiwa ufumbuzi wa moja kwa moja, makampuni ya biashara yaanzishe au kushiriki katika taratibu madhubuti za kushughulikia malalamiko katika ngazi ya uendeshaji kwa ajili ya watu binafsi na jamii ambazo zinaweza kuwa zimeathirika vibaya.

Maoni

Taratibu madhubuti za kushughulikia malalamiko katika ngazi ya uendeshaji zinapatikana moja kwa moja kwa watu binafsi na jamii ambazo zinaweza kuwa zimeathirika kuokana na matendo ya kampuni ya biashara. Kwa kawaida husimamiwa na makampuni ya biashara peke yake au kwa kushirikiana na watu wengine, ikiwa ni pamoja na wadau husika. Zinaweza pia zikatolewa kwa makubaliano na mtaalam au chombo nje ya kampuni. Haihitajiki kwamba wale wanaoleta malalamiko watumie kwanza njia nyingine za kupata msaada. Walalamikaji wanaweza kushirikisha kampuni ya biashara moja kwa moja katika kutathmini masuala hayo na kutafuta ufumbuzi wa madhara yoyote.

Taratibu za ngazi za uendeshaji malalamiko zilizo madhubuti hutekeleza kazi mbili muhimu kuhusu wajibu wa makampuni ya biashara kuheshimu haki za binadamu.

- Kwanza, wanaunga mkono utambuzi wa athari mbaya kwa haki za binadamu kama sehemu ya juhudi endelevu zinazostahili za kampuni, juu ya athari mbaya kwa haki za binadamu. Hufanya hivyo kwa kutoa fursa kwa wale walioathirika moja kwa moja na shughuli za kampuni kuelezea matatizo wanapoamini kuwa wanaathirika au wataathirika vibaya. Kwa mwenendo na muundo wa uchambuzi katika malalamiko, makampuni ya biashara yanaweza pia kutambua matatizo ya mfumo na kuchukua hatua ipasavyo;
- Pili, taratibu hizi huwezesha malalamiko kushughulikiwa mara yanapotambuliwa, na athari mbaya kutafutiwa ufumbuzi mapema na moja kwa moja na makampuni ya biashara, na hivyo kuzuia madhara yasiwe mabaya zaidi na malalamiko yasiendelee.

Taratibu kama hizi hazihitaji kungoja hadi malalamiko au kero zifikie kiwango cha madai ya ukiukwaji wa haki za binadamu kabla ya kuelezewa, bali hasa zina lengo la kubainisha masuala yoyote halali ya wale ambao wanaweza kuwa wameathirika vibaya. Ikiwa matatizo hayo hayatambuliwi wala kushughulikiwa, baada ya muda yanaweza kuwa migogoro mikubwa na ukiukwaji zaidi wa haki za binadamu.

Taratibu za kushughulikia malalamiko zilizo katika ngazi ya uendeshaji lazima ziwe na vigezo fulani ili kuhakikisha zinakuwa na ufanisi katika utendaji wake (Kanuni ya 31). Vigezo hivi vinaweza kutimizwa kwa kuzingatia mambo mbalimbali katika taratibu za kushughulikia

malalamiko kwa mujibu wa mahitaji ya ukubwa, rasilimali, sekta, utamaduni na vigezo vingine.

Taratibu za kushughulikia malalamiko zilizo katika ngazi ya uendeshaji zinaweza kuwa njia muhimu ya ushiriki mpana wa wadau na michakato ya majadiliano ya pamoja, lakini haziwezi kuwa mbadala wa yote. Taratibu hizo zisitumike kudhoofisha majukumu ya vyama halali vya wafanyakazi katika kushughulikia migogoro ya kikazi, wala kuzuia upatikanaji wa huduma ya mahakama au taratibu nyingine zisizokuwa za kimahakama za kutolea malalamiko.

30. Viwanda, wadau mbalimbali na mipango mingine shirikishi inayotokana na kuheshimu misingi ya haki za binadamu inapaswa kuhakikisha kuwa kuna uwepo wa taratibu madhubuti za kushughulikia malalamiko.

Maoni

Viwango vinavyohusiana na haki za binadamu vinazidi kujitokeza katika wajibu wakuvizingatia kwa makampuni, wadau mbali mbali na mipango mingine ya ushirikiano, kwenye kanuni za maadili, viwango vya utendaji, makubaliano ya mfumo ya kimataifa kati ya vyama vya wafanyakazi na makampuni ya kimataifa ya biashara, na shughuli kama hizo zinazofanana.

Mipango hiyo shirikishi inapaswa kuhakikisha zipo taratibu zenye ufanisi ambazo walioathirika au wawakilishi wao halali wanaweza kuwasilisha matatizo wanapoamini kuwa ahadi zilizotolewa hazikutimizwa. Uhalali wa taratibu za mipango unaweza kuwekwa hatarini kama hamna hizo taratibu. Taratibu hizo zinaweza kuwa katika kiwango cha mtu binafsi, mipango shirikishi, au vyote viwili. Taratibu

hizo zinapaswa kutoa uwajibikaji na kusaidia kuwezesha urekebishaji wa athari mbaya kwa haki za binadamu.

VIGEZO VYA UFANISI KWA TARATIBU ZISIZO ZA KIMAHAKAMA ZA KUSHUGHULIKIA MALALAMIKO

31. Taratibu za kushughulikia malalamiko, za serikali na zisizo za serikali ili kuhakikisha ufanisi wake zinatakiwa ziwe:

- (a) Halali:** Kuweka imani kwa makundi ya wadau waliokusudiwa, na kuwajibika kwa utendaji wenye usawa katika michakato ya malalamiko;
- (b) Kufikika:** kujulikana kwa makundi yote ya wadau ambao matumizi yake yamekusudiwa, na kutoa misaada ya kutosha kwa ajili ya wale ambao wanaweza kukabiliwa na vikwazo fulani katika kufikia taratibu hizo;
- (c) Kutabirika:** kutoa utaratibu wa wazi na unaojulikana, wenye kipindi cha muda wa utekelezaji kinachoonyesha kila hatua, na uwazi juu ya aina za mchakato na matokeo yanayopatikana na njia za kufuatilia utekelezaji;
- (d) Usawa:** zinazohakikishakwambapandezinazotofautiana zinapata vyanzo vya habari vya kuridhisha, ushauri na utaalamu muhimu wa mchakato wa malalamiko wa haki, wenye taarifa na heshima;
- (e) Uwazi:** kuzifahamisha pande husika maendeleo ya malalamiko, na kutoa taarifa za kutosha kuhusu utendaji wa utaratibu huo, ili kujenga imani katika kuleta ufanisi wake na kutimiza maslahi yoyote ya umma yaliyo hatarini;

(f) Haki sawa: kuhakikisha kwamba matokeo na ufumbuzi vinaendana na haki za binadamu zinazotambuliwa kimataifa;

(g) Chanzo cha mafunzo endelevu: kuchukua hatua muhimu za kutambua mafunzo ya kuboresha utaratibu huo na kuepuka malalamiko na madhara ya baadaye;

Taratibu za ngazi za uendeshajizinaswa pia:

(h) Kutokana na ushiriki na mazungumzo: ushauri wa vikundi vya wadau kwa ajili ya wale waliokusudiwa kutumia muundo na utendaji wake, na kulenga katika mazungumzo kama njia ya kukabiliana na kutatua malalamiko yao.

Maoni

Utaratibu wa kushughulikia malalamiko unaweza tu kutimiza malengo yake kama watu waliokusudiwa kuutumia wanaujua, wanaimani nao na wanaweza kuutumia. Vigezo hivi vinatoa viwango vya utayarishaji,, urekebishaji au utathmini wa utaratibu wa kushughulikia malalamiko usiokuwa wa kimahakama ili kuhakikisha kwamba utekelezaji wake unaleta manufaa. Taratibu za kushughulikia malalamiko zilizoundwa au kutekelezwa kihafifu zinaweza kusababisha mchanganyiko wa hisia za kero miongoni mwa wadau walioathirika kwa kuzidisha hisia zao za mchakato kutowapa madaraka na kutowaheshimu.

Vigezo saba vya kwanza vinahusu utaratibu wowote wa Serikali au usio wa Serikali, wa uamuzi wa kimahakama au wa mazungumzo. Kigezo cha nane ni maalum kwa taratibu za kushughulikia malalamiko katika ngazi za uendeshaji ambazo makampuni ya biashara husaidia kusimamia.

Istilahi “utaratibu wa kushughulikia malalamiko” hapa limetumika kama neno la kiufundi. Istilahi yenyewe inaweza isiwe sahihi au ya kufaa wakati wote inapotumika kwenye utaratibu maalum, lakini vigezo vya ufanisi vinabaki vilevile. Yafuatayo ni maoni juu ya vigezo maalum:

- (a) Wadau ambao wamekusudiwa kwa matumizi ya utaratibu huu lazima wawe na imani nao iwapo wameamua kuutumia. Uwajibikaji kwa kuhakikisha kwamba pande zinazohusika na mchakato wa malalamiko haziingilii kati mwenendo wake wa haki ni jambo muhimu kabisa katika kujenga imani kwa wadau;
- (b) Vikwazo vya ufikiwaji ni pamoja na kutokupata taarifa juu ya utaratibu na kutofahamu utaratibu wenyewe, lugha, kusoma na kuandika, gharama, mahali na hofu ya kuadhibiwa;
- (c) Ili utaratibu uaminike na kutumika, unapaswa kutoa taarifa kwa umma kuhusu utaratibu inaofuata. Kipindi cha muda wa utekelezaji kwa kila hatua kinapaswa kuheshimiwa kila inapowezekana, kwa kukubali kwamba wakati mwingine kunahitajika utayari wa kubadilika;
- (d) Katika malalamiko au migogoro kati ya makampuni ya biashara na wadau walioathirika, wadau hao mara kwa mara hukosa taarifa na wataalam, na mara nyingi hukosa fedha za kuzilipia. Kutorekebisha hali hii ya kutokuwa na usawa huweza kupunguza mafanikio na mtazamo kuwa mchakato ni wa haki na kuleta ugumu kupata ufumbuzi wa kudumu;
- (e) Kuwasiliana mara kwa mara na pande husika kuhusu maendeleo ya ushughulikiaji malalamiko ya mtu binafsi inaweza kuwa muhimu kwa ajili ya kudumisha imani ya mchakato. Kuweka uwazi wa kiutendaji wa utaratibu kwa wadau

mbalimbali, kwa njia ya takwimu, maeneo ya uchunguzi au maelezo zaidi kuhusu ushughulikiaji wa baadhi ya kesi, inaweza kuwa muhimu ili kuonyesha uhalali wake na kudumisha imani zaidi. Wakati huo huo, usiri wa mazungumzo kati ya pande hizo na utambulisho wa mtu binafsi unapohitajika unapaswa kutolewa;

- (f) Malalamiko mara nyingi hayaandaliwi kwa kigezo cha haki za binadamu na mengi mwanzoni hayataji suala la haki za binadamu. Licha ya hayo, matokeo yanapokuwa na athari kwa haki za binadamu, inabidi kuwepo uangalifu ili kuhakikisha kwamba zinaendana na haki za binadamu zinazotambuliwa kimataifa;
- (g) Uchambuzi wa mara kwa mara wa marudio, mienendo, aina na sababu za malalamiko unaweza kuziwezesha taasisi zinazosimamia utaratibu kutambua na kushawishi sera, taratibu au utendaji ambao unapaswa kubadilishwa ili kuzuia madhara ya baadaye;
- (h) Kwa utaratibu wa kushughulikia malalamiko katika ngazi ya uendeshaji, kushirikisha makundi ya wadau walioathirika katika mpango na utendaji wake kunaweza kusaidia hukidhi mahitaji yao, kwamba watatumia kwa vitendo na kuwa kuna maslahi ya pamoja kuhakikisha mafanikio yake. Kwa kuwa kampuni ya biashara haiwezi, kihalali, kuwa ndiomsababisha malalamiko na kwa upande mmoja kuwa muamuzi wa matokeo ya hayo malalamiko, taratibu hizi zinapaswa kuzingatia kufikiwa kwa ufumbuzi wa makubaliano kwa njia ya mazungumzo. Pale ambapo hukumu itahitajika, inapaswa itolewe na mfumo halali, huru wa mtu wa tatu.